# UTAMADUNI WA MZANZIBARI: MILA NA DESTURI KATIKA VAZI LA KANGA

*Saade S. Mbarouk* na *Ulfat A. Ibrahim*

**Ikisiri**

Makala hii inaangazia matumizi ya vazi la kanga katika mila na desturi katika utamaduni wa Mzanzibari. Kila jamii huwa na kaida zake ambazo hutofautiana na jamii nyingine. Kaida hizo huwa katika chakula, mavazi, pamoja na mfumo mzima wa maisha. Lengo la makala hii ni kubainisha kwa namna gani Wazanzibari wanavyotumia kanga kulingana na mila na desturi zao. Matumizi hayo huwa katika hatua mbalimbali za makuzi ya mwanadamu, kuanzia kuzaliwa kwake, kuishi na kufa kwake. Makala hii ni sehemu ya utafiti mkubwa uliofanywa na Saade Mbarouk (2011) ambao unahusu Athari za Semi za Kanga kwa Jamii ya Zanzibar. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano. Nadharia ya Naratolojia imetumika katika kuchambua data. Katika makala hii waandishi wameeleza fasili ya kanga, aina za kanga, asili ya jina la kanga pamoja na historia ya kanga. Mwisho, wameelezea umuhimu wa kutunza utamaduni wa jamii.

## Utangulizi

Makala hii inahusu mila na desturi zinazotumika kwenye kanga katika jamii ya Zanzibar. Zanzibar ni visiwa vilivyomo katika Bahari ya Hindi. Miongoni mwa visiwa hivyo, viwili ndivyo vikubwa, yaani Unguja na Pemba. Kwa upande wa Magharibi, visiwa hivyo vimepakana na mwambao wa Tanzania Bara. Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kisiwa cha Unguja kipo umbali wa kilomita 40 Mashariki ya Bagamoyo, Tanzania Bara. Watu wake wengi huishi katika sehemu za Kaskazini, Magharibi na Kati ambako kuna rutuba kwa kilimo. Sehemu za mwambao ni nzuri kwa shughuli za uvuvi pamoja na biashara za utalii na matembezi katika fukwe nzuri (https://www.tanzaniatourism.go.tz/en/destination/zanzibar-island).

Kama ilivyo sehemu yoyote ile ya nchi, Zanzibar ina utamaduni wake ambao, kwa kiasi fulani, unatofautiana na maeneo mengine ya Tanzania, hasa upande wa mapishi na mavazi. Utamaduni huo umeathiriwa kwa kiasi kikubwa na wageni kutoka sehemu za bara Arabu na Asia. Tukiangalia upande wa mavazi, wanawake wengi wa Zanzibar huvaa kanga.

Kanga ni vazi maalumu lenye umbo la pembe nne ambalo hunakshiwa kwa rangi, maua au michoro tofauti yenye kuvutia. Kanga hubuniwa katika mtindo mahsusi wa kuwa na pindo, pia upande wa chini wa mji katikati huwekwa semi mbalimbali.

Kanga huwa na urefu wa karibu mita mbili na hutengenezwa kwa mtindo wa doti (pande mbili). Aghalabu, huvaliwa na wanawake kwa kujifunga kiunoni au kifuani upande mmoja, upande wa pili hujitanda kichwani na huporomokea hadi mabegani na mgongoni (Mbarouk, 2011).

Inasemekana kuwa vazi hili limekuwa likitumiwa katika mwambao wa Afrika Mashariki tokea karne ya kumi na tisa. Mara nyingi kanga huandikwa semi kama vile methali, mafumbo na misemo ambayo hubeba ujumbe ndani uliojikita katika maisha ya mwandamu ikiwa ujumbe wa kijamii, kisiasa na kidini. Inasemekana kuwa mwanzo semi hizo ziliandikwa kwa hati za Kiarabu (Zawawi, 2007). Siku hizi, kanga nyingi huandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kutumia hati ya Kirumi.

**Nadharia ya Utafiti ya Usimulizi**

Prince (1987) ananukuliwa na Wamitila (2004) akielezea simulizi kama uelezaji wa tukio moja au mengi ya kihalisi au kibunilizi… tokeo, njia, lengo na tendo, muundo na uundaji wake. Vilevile, Genette (1980) anaieleza dhana hii ya Naratalojia kwa kurejelea mambo matatu tofauti. Kwanza, kuelezea kauli ya kisimulizi au kimaandishi au isiyo ya kimaandishi iliyodhamiriwa kulieleza tukio au matukio fulani. Pili, mfuatano wa matukio halisi au kibunilizi ambayo ni kiini au yanalengwa na usemi fulani. Na, tatu, kuelezea tendo lenyewe la kusimulia au usimuliaji.

Makala hii imetumia nadharia ya Usimulizi (Naratolojia) katika ukusanyaji wa data, uchambuzi na hata uwasilishaji wake. Nadharia hii inatilia mkazo muktadha wa kijamii kwa kuzingatia usimulizi na hadhira yake. Kutokana na muelekeo huo, imeweza kusaidia katika simulizi juu ya matumizi ya kanga kwa mujibu wa jamii ya Zanzibar. Kwani simulizi hizo zinatokana na matukio halisi ya wanadamu. Pia, hutokea katika miktadha tofauti ya kijamii. Kwa hivyo, nadharia hii ni muhimili mzuri katika kuchambua na kuwasilisha data za utafiti huu. Kupitia nadharia hii, waandishi wamechambua masimulizi kwa upana kutoka kwa watafitiwa pamoja na matini mbalimbali.

**Dhana ya Kanga: Maana, Historia, Aina, na Maendeleo Yake**

Watu mbalimbali wametoa maana ya kanga kwa kutumia vigezo tofauti kama vile ukubwa wa nguo yenyewe, malighafi iliyotumika, na hata mtindo wa upangaji wa nakshi zake. Kwa mfano, Othman (1997) anasema:

> Kanga is a piece of printed cotton fabric about 1.5m by 1m, with a border along all the four sides (called pindo in Kiswahili) and a central part (mji) of different design from the border. It is designs like any other fabric.

Kanga ni kipande cha kitambaa cha pamba kilichonakshiwa chenye ukubwa wa 1.5m kwa 1m kilichozungushiwa pindo pande zote nne na sehemu ya kati (mji) wenye nakshi tofauti kutokana na pindo. Hunakshiwa kama nguo nyingine yoyote (Tafsiri yetu).

Vilevile, Kirknxs (2005) ameeleza maana ya kanga kwa kuzingatia vigezo vya umbo (*size*), sanaa na utamaduni. Anasema: "*Kanga, a simple printed piece of cotton measuring 115 x 170cm, embodies art, beauty, culture and customs of coastal women.*" Anamaanisha kuwa, "Kanga, kipande cha nguo cha pamba cha kawaida chenye kipimo cha 115 x170 cm, chenye kuwakilisha sanaa, uzuri, utamaduni na mila za wanawake wa pwani (Tafsiri yetu). Ifuatayo ni picha inayoonesha namna kanga zinavyovaliwa na watu wanapokuwa katika shughuli za miviga kama vile, mazishi, maulidi, na harusi ya kanga, pamoja na katika shughuli za kijamii kama vile mikutano.



Picha Na. 1: Vazi la kanga (lughatatu.wordpress.com).

Ingawa watafiti wameandika juu ya umbo au ukubwa wa kanga kwa kuonesha vipimo mbalimbali, lakini umbo la kanga hutegemea kiwanda au sehemu zilimotengenezwa. Kwa mfano, kanga zilizotengenezwa Oman huweza kutofautiana na zile zilizotengenezwa India. Mara nyingine, hata ndani ya nchi moja, kama vile Tanzania, kanga zilizotengenezwa na kiwanda cha Urafiki hutofautiana na kanga za kiwanda cha *Karibu Textile Mills* (KTM).

Hanby na Bygott (1984) wanaeleza kuwa, asili ya kanga ni Waswahili wa mwambao wa Afrika Mashariki, hususani Zanzibar mnamo karne ya kumi na tisa. Wataalamu hao walipingwa na Troughear (1984) ambaye ameeleza kuwa, Zanzibar ni sehemu ambayo mfanyabiashara maarufu mwenye asili ya India aliiga ubunifu huo wa kutoka Mombasa. Hivyo basi, kwa haraka alibuni huo mtindo wa vipande sita vya leso na kufanya kipande kimoja ambao umekuwa maarufu hadi leo.

Kuhusu asili ya jina 'kanga', Zawawi (2007) ameeleza kuwa, katika karne ya kumi na tisa, baadhi ya wanamitindo wa kike wa Zanzibar walinunua vitambaa vya kufutia mkono vilivyotengenezwa kwa pamba, vyenye urefu wa inchi sita (6) na kuviunganisha pamoja na baadaye walivikata vipande viwili na kuvifanya vya kipekee. Mtindo mwingine mpya uliitwa leso. Leso ilipata umaarufu wa haraka kuliko aina nyingine za nguo za nakshi zilizopatikana. Kabla ya wabunifu wa biashara wa mwambao wa Afrika Mashariki kutoa mtindo maalumu uliochapishwa, wenye vipande sita vya leso vilivyo pamoja kama ni nguo moja. Mtindo huu mpya ulikuwa na pindo na nakshi za vidoadoa vyeupe katika mji mweusi. Hivyo, wauzaji na jamii kwa haraka walitoa jina la "kanga" kutokana na kufananisha mji na umbile la kuvutia la rangi za ndege aina ya kanga, ambayo ni nyeusi kwa vidoti vyeupe.

Zawawi (2007) ananukuliwa na Shadow (2010) akieleza kauli inayodai kuwa, asili ya kanga (leso) ilikuwa ikihusishwa na aibu ya biashara ya utumwa. Inasemekana kuwa, watumwa wa kike mnamo karne ya 19 walikuwa wakivaa nguo maalum kabla ya kusafirishwa kupelekwa nchi za Mashariki ya Kati. Aina ya nguo zilizotumika zilikuwa ni kaniki. Walipewa nguo hizo kutokana na masharti ya kidini ya Kiislamu. Wafanyabiashara hao waliona kuwa vazi la kaniki (kanga) ndio hasa linalofaa kutokana na shughuli hiyo. Kutokana na fikira hizo, wafanyabiashara kutoka Gujurat huko Bara Hindi, ambao walifanya ziara katika Mwambao wa Afrika Mashariki, walibaini kuwa kulikuwa na mahitaji ya soko la aina ya nguo hizo (kaniki). Hivyo, walichangamkia biashara hiyo kwa haraka. Walisambaza nguo hizo nyeusi zilizoitwa kaniki, ambazo walivaa masikini na watumwa wanawake.

Maendeleo kuhusu vazi hilo (kanga) yalijitokeza kadiri ya siku zilivyosonga mbele. Nakshi nyingine katika kaniki ziliwekwa. Nakshi ya mwanzo iliyobuniwa ilikuwa mfano wa umbo la muhogo au viazi vitamu. Nakshi hizo zilichapishwa katika mji mweusi wa kaniki na nguo nzima. Maumbo hayo yalikuwa ya rangi nyeupe. Wanawake waliovaa nguo hizo walipokuwa wakijikusanya na kuzungumza wakati wa jioni na katika fukwe za Zanzibar, walifananishwa na ndege aina ya kanga. Hii ni kutokana na muonekano wa rangi za nguo hizo. Kutokana na sababu hiyo, nguo hizo zilianza kuitwa jina la "kanga" (Shadow, 2010).

Kadiri siku zilivyoendelea, kanga zilianza kupata mitindo mbalimbali. Inasemekana kuwa, wanawake walioachwa huru kutokana na utumwa kutoka mwambao wa Afrika Mashariki na Zanzibar, pamoja na wanawake wengine katika maeneo mengine, walihitaji mabadiliko ya mitindo ya kanga. Hivyo, walifanya majadiliano na kufanya kanga kuwa ni mtindo mahsusi katika karne ya ishirini. Muonekano wa kanga ulizidi kubadilishwa kadiri siku zilivyokwenda. Ujumbe wa kimaandishi na methali ni miongoni mwa mabadiliko ya muonekano wa kanga.

Mabadiliko hayo yalifanywa na familia maarufu ya Hajee Essak aliyejulikana kama Abdallah. Huyu, asili yake ni Zanzibar lakini alihamia Mombasa mnamo 1910. Kanga zake zilijitofautisha kwa nembo iliyoandikwa "K.H.E Mali ya Abdallah" pamoja na maandishi yaliyojumuisha semi kama vile methali. Lugha iliyokuwa ikitumika ilikuwa ni Kiswahili, na hati zilizotumika zilikuwa ni za Kiarabu. Tuanafikiria kuwa, maelezo haya ndiyo yaliyozaa mtazamo kuwa asili ya kanga ni Zanzibar. Hata hivyo, baada ya kufahamika na kuenea kwa hati za Kirumi katika Afrika Mashariki, semi za kanga zilianza kuandikwa kwa herufi za Kirumi. Hali ambayo imezoeleka zaidi hivi sasa.

Kabla ya India kuwa kiongozi katika viwanda vya kanga, mashine za kutengeneza kanga zilitokea nchi za Ulaya na China. Baada ya hapo, viwanda vya kanga vilianzishwa pia katika nchi za Afrika Mashariki, kama vile Kenya na Tanzania. Hata hivyo, ingawa India ni miongoni mwa nchi zenye kutengeneza kanga na kuziuza katika pande mbalimbali ulimwenguni, vazi hili huwa halivaliwi huko. Hali hii inatokana na sababu kuwa, kwa muda mrefu fikra kuhusu nguo hizo huko India zinafungamanishwa na wazo la utumwa.

Kutokana na maendeleo hayo, mitindo mipya ya kanga ilijitokeza. Mitindo hiyo ilihusisha yenye nakshi rahisi na nakshi za mchanganyiko. Aidha, zilijumuishwa picha za vitu vyenye dhamira au taswira za majumbani (kama vile kuku) na mazao mbalimbali (kama vile ndizi na karanga). Zaidi, zilinakshiwa kwa picha za maumbo ya maumbile ya kuvutia kama milima, mwezi, maua, nyota, na majengo ya kihistoria. Hali hiyo yamabadiliko imeendelea kadiri jamii inavyobadilika kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi. Mbali ya picha na nakshi, kanga hupata mvuto zaidi pale zinapobeba ujumbe maalumu. Mchanganyiko huu hukamilisha upekee wa vazi hili. Zawawi (2007) anatilia mkazo kuhusu jambo hili la mvuto kwa kusema kuwa, mtindo ulio maarufu zaidi wa kuleta mvuto ni ule wa matunda au vitu vya nyumbani au maumbo. Anaongeza kuwa, kanga hupata jina lake la kwanza la jumla (*its generic name*) kutokana na kitu kilichowasilishwa au kuchorwa.

Aina za kanga hujitokeza kutokana na tofauti za maumbile yake kama vile ukubwa, uzito, semi na malighafi iliyotengenezewa. Kutokana na vigezo hivyo, tunapata aina tofauti za kanga. Kumekuwa na kanga nzito na kanga nyepesi, kanga kubwa na kanga za kawaida, kanga za majina na kanga bubu (yaani kanga zisizo na semi ya aina yoyote). Vilevile, aina hujitokeza kutokana na pahala zilikotengenezwa au muagizaji wa kanga hizo. Mfano, kanga za India, kanga za Mombasa na kanga za Chavda.

Mbali na jina la jumla, jina mahususi la kanga hutokana na umbo la kanga (picha), jina (semi), rangi au nakshi yake. Ni jambo la kawaida kwa kanga kupewa jina kulingana na kile kilichojitokeza zaidi; hivyo, kubeba dhima kuu kanga hiyo. Hata hivyo, mara nyengine huweza kupata majina kutokana na jina na picha, au kutokana na picha au mchoro na rangi Zawawi (2007). Kuhusu picha, kanga huweza kupata jina kutokana na picha zilizo katika mitindo mbalimbali (Zawawi, 2007). Inawezekana picha ikawa katikati, na baadaye picha hiyohiyo ikajitokeza sehemu ya pindo. Au picha moja kubwa ikawekwa katika duara katikati na kwenye pindo kukajitokeza nakshi nyingine. Vilevile, picha au maua ya aina fulani huweza kujitokeza mji mzima. Mathalani, kanga yenye picha ya bata ikiwa atachorwa kwa mitindo tofauti, kama vile kuwekwa katika duara, katikati ya kanga, au wamechorwa mji mzima wa kanga, itaitwa kanga ya bata. Aina nyingine ya picha ni kama vile ya mnazi, mwembe, mchungwa, asumini, muhindi, pilipili na kadhalika. Hata hivyo, kuna ambazo hutumia majina mawili, yaani kwa kutumia picha na jina (semi) kwa wakati mmoja. Mfano mzuri ni kanga za asumini, hujulikana kwa jina la "Alaa Kumbe" na "Asumini". Mfano mwengine ni kanga ya bata, hujulikana kwa jina la kanga za bata na "Kila uonalo wasema..."

Kanga nyingine ambazo ni maarufu kutokana na maumbo yaliyochorwa ni kanga za kisutu. Kanga hizi huwa na nakshi na alama za maumbo ya kihesabu. Kama alama ya jumlisha na alama zero. Mara nyingi nakshi hizo huenea katika mji mzima wa kanga, na katika pindo nakshi zinakuwa ni tofauti na hizo. Kanga hizi hutengenezwa katika rangi tofauti kama vile bluu kwa weusi, nyekundu kwa weusi (kisutu cha bi harusi), nyekundu, nyeupe na weusi, au manjano kwa kijani. Kanga hizi ni maarufu sana Visiwani Zanzibar, hasa katika mazingira ya harusi na katika sherehe za kijamii na serikali ambako huvaliwa kama sare au hushonwa kanzu (Mbarouk, 2011). Mfano wa kanga za kisutu umetolewa katika picha ya hapo chini:



Picha Na. 2: Kanga ya kisutu chekundu (kabatilakanga.wordpress.com).

Mfano mwingine ni kanga ya mnazi, ambayo ni maarufu kwa kuwa na picha ya mnazi katika kanga hiyo kama inavyoonekana katika picha inayofuata.



Picha Na. 3: Kanga ya Mnazi (kabatilakanga.wordpress.com).

Rangi kutoa jina katika kanga ni kitu kilichozoeleka sana katika vazi hili. Kanga maarufu ambazo zimepewa jina kutokana na rangi ni kanga za Magharibi. Kanga hizi ni zile zenye rangi ya bluu iliyotia kiza na nakshi za rangi nyeusi, hata kama zitakuwa na picha au nakshi tofauti. Huitwa kanga za Magharibi kutokana na kubeba dhana ya wakati wa Magharibi, wakati ambao jua linamalizia kuzama na kiza au weusi wa usiku unaingia; na wakati huo huo, kuyadhoofisha mawingu ya bluu yasioneshe dhahiri rangi yake ya samawati. Hii ni kwa sababu mchanganyiko wa rangi nyeusi kwa bluu huwa na kiza kidogo. Na ndiyo maana kanga hizo zikapewa jina la "kanga za Magharibi". Kwa mfano, kanga moja ina nakshi ya korosho na nyingine ina picha ya mwamvuli, kwa vile zote zina rangi hizo, huitwa kanga za Magharibi (Mbarouk, 2011).

Hata hivyo, kuna kauli nyingine inayotofautiana kidogo na rangi zilizoelezwa mwanzo. Kwa mujibu wa Bi Nassra[7], kanga za mwanzo za Magharibi zilikuwa na rangi ya zambarau iliyokoza sana ambayo ilizifanya hata zile nakshi nyeusi zilizochorwa katika kanga zisionekane vizuri. Sio bluu na weusi zilizozoeleka kuitwa hivi sasa. Mifano mingine ni kanga za moto ambazo ni zenye rangi

[7] Ni mwandishi wa habari wa zamani wa Sauti ya Zanzibar, pia ni mtaalamu wa mambo ya utamaduni wa Zanzibar. Aliyasema hayo nyumbani kwake Malindi Zanzibar wakati wa mahojiano yake na Mbarouk tarehe 20 Julai 2010.

nyekundu kwa weusi, kanga za mrututu zenye rangi nyeusi na bluu, kanga za rangi ya poda, na rangi ya malai[8].

Vilevile, kuna kanga za sharubati. Kanga hizi rangi yake ni wardi iliyokoza sana. Mfano wake ni kama kinywaji kilichokuwa maarufu visiwani Zanzibar kinachoitwa sharubati. Mara nyingi kanga za sharubati, rangi zake hujitokeza zaidi katika mji mzima na katika pindo. Rangi hiyo huzifanya kanga ziwe zenye kung'ara na kuvutia sana machoni. Hivyo, hupewa jina hilo kutokana na kuwa, rangi hiyo hujitokeza zaidi na kuzivuta hisia za watazamaji kushinda zile nakshi zilizochorwa katika kanga hiyo (Mbarouk, 2011).

**Mila katika Kanga**

Kanga ziliendelea kupata sifa kadiri siku zilivyoendelea hadi kuwa vazi la utamaduni na kutumika katika mila na desturi mbalimbali za Kizanzibari. Kama ilivyoelezwa na Zawawi (2007), kanga katika mila na desturi za Wazanzibari hutumika kuanzia siku ya kuzaliwa hadi siku ya kufa.

**Kanga Wakati wa Kuzaliwa Mtoto**

Katika jamii ya Wazanzibari, kanga huanza kutumika mara tu pale mtoto anapozaliwa kwa kufunikwa, kabla ya kuvalishwa aina yoyote nyingine ya nguo. Hii inatokana na itikadi kuwa, mtoto anapovalishwa kanga mpya anapozaliwa huwa na bahati ya kupendwa na watu. Kinyume chake, kuvalishwa kanga iliyochakaa ni kumtia mkosi au nuhusi. Mtoto anaweza kuvalishwa kanga kwa kufunikwa na pengine hadi siku ya pili ndipo hutafutiwa nguo nyingine na kuvalishwa. Hata hivyo, kanga huendelea kutumika kwa mtoto huyo kwa matumizi kama kumbebea, kumtandikia sehemu yake ya kulala na hata kumfunga anapomaliza kuoga. Zaidi, hutumika kumfunga kama nguo ya ndani kwa ajili ya kuzuia kutapakaa kwa haja kubwa na ndogo.

Licha ya mila hizo, vuguvugu la mabadiliko katika jamii kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia yanapoteza baadhi ya mila katika jamii ya Zanzibar. Haya yanadhihirika pale ambapo baadhi ya wauguzi wanapokataza wazazi wanapokwenda kujifungua kuchukua kanga mpya kutokana na kuhofia kanga kuwa na maambukizi yanayoweza kumdhuru mtoto. Msimamo wa makala hii kuhusu hoja hiyo yenye mwegamo wa kiafya ni kwamba, ni nguo hiyo iendelee kuruhusiwa kutumika kwa shabaha hiyo; bali ni vyema ifuliwe japo mara moja ili kuiweka

[8] Ni aina ya viburudisho ambavyo hutengenezwa kwa kutumia sharubati ya matunda mbalimbali na kugandishwa katika jokofu. Hapo zamani malai yakitengezwa kwa kutumia sharubati maalumu ambayo iliifanya kuwa na muonekano wa rangi nyekundu yenye mchanganyiko na rangi ya kahawia.

katika usafi wa kuaminika kabla ya kumfunika mtoto. Ifahamike kuwa jambo hili lilikuweko tokea zamani. Wazee walikuwa wakifua kanga kwa maji matupu kabla ya kuanza kuzivaa. Hii ina maanisha kuwa hata inapotumika kwa kumvisha mtoto anapozaliwa inakuwa tayari imepata angalau fuo moja. Yumkini, hali hiyo ilipotea kutokana na vijana wengi kutoelewa maana na thamani ya kufanya hivyo.

**Vazi la Kanga wakati wa Kubalehe**
Kanga huchukua nafasi muhimu kwa mtoto wa kike anapobalehe. Mama mzazi wa mtoto huyo hulazimika kupeleka kanga kwa somo. Somo huyo hufanya wajibu wake wa kutoa mafunzo ya namna ya kutumia kanga katika kukabiliana na yale mabadiliko ya kimaumbile yanayomtokezea pamoja na kujistiri mwili. Kanga pia hutolewa na somo kama zawadi kwa mwari wake. Kwa upande wa wavulana, katika miaka ya nyuma, kanga zilitumika kwa mtoto wa kiume walipokuwa jandoni. Alivalishwa kanga katika kipindi chote cha kupelekwa jandoni hadi anapomaliza muda huo. Hii ni kwa sababu kanga ni nyepesi hazina joto. Hivyo, mama humvalisha mtoto wake ili kumstiri bila kujitonesha.

**Kanga katika Muktadha wa Ndoa**
Mbali ya matumizi hayo yaliyoelezwa, kanga inabeba nafasi mahsusi katika muktadha wa ndoa. Katika muktadha huu, kanga huchukuwa nafasi kabla na ndani ya ndoa. Kabla ya harusi, miongoni mwa matayarisho ya harusi kwa pande zote mbili ni kutafutwa kanga kwa ajili ya bibi harusi.

Kwa upande wa mume, kuna kanga ambazo hununuliwa na kuwekwa katika sanduku maalum ambalo hukabidhiwa bibi harusi. Sanduku hili hupewa akiwa pamoja na watu wake wa karibu baada ya kufunga ndoa. Ingawa mnakuwa na vitu vingine, kwa kawaida, kanga huchukuwa nafasi kubwa zaidi. Kama alivyothibitisha Bi Nassra wakati wa mahojiano na watafiti kuhusu umuhimu wa matumizi ya kanga katika muktadha huu amesema, "kanga ndio fahari ya sanduku". Kwa upande wa bibi harusi, mama wa bibi harusi na somo hununua kanga kwa ajili ya mtoto wao. Katika ununuzi huo, majina mazuri ni kitu kinachozingatiwa. Inapokaribia harusi, kanga hizo hutayarishwa vizuri kwa kumwagiwa marashi, asumini, kufukizwa udi, pamoja na kuwekewa manukato mengine (kuvumbikwa) kwa ajili ya kutumika siku za fungate. Kwani ni aibu kutegemea kanga zinazotoka kwa mume, hasa katika kipindi hicho.

Ndani ya ndoa kanga hutumika kama chombo cha mawasiliano. Wanandoa huweza kuwasiliana kupitia semi zilizo katika kanga. Kanga zenye ujumbe teule unaoendana na mahitaji husika huvaliwa na mke akiwa nyumbani kwake. Kanga hutoa ujumbe kwa mume au kwa mke bila ya mmoja wao kuinua mdomo. Vilevile, kanga hutumika chumbani kwa kutandikwa juu ya kitanda na kuwekwa ujumbe huo vizuri ili uonekane na mhusika. Mtindo huu wa kutandika kanga juu ya kitanda,

kwa kiasi kikubwa, unatoweka kwa sasa kama si kupotea kabisa. Mifano ya jumbe hizo ni: “Tulia tuishi wazuri haweshi”, “Wapendanao hufarijiana”, “Mapenzi ni jeraha nipende nione raha”, “Kuishi ni kuvumiliana”, “Mapenzi ya ndoa ni matamu hayanishi hamu”, “Bwana nipe wiki kazi na njaa haifanyiki”, na “Ukinienzi nitakuenzi nitazidisha mapenzi”.

Mbali ya kanga za aina tofauti anazopewa bibi harusi katika muktadha huu wa ndoa, kuna kanga maalum ambazo huvishwa maharusi (bibi harusi); mara nyingi, huwa kanga za kisutu.

**Upekee wa Kanga za Kisutu**

Kanga za kisutu ambazo ni maalumu kwa ajili ya kuvaa maharusi zilipoanza kutoka zilikuwa ni za rangi mbili tu. Kisutu cha bibi harusi ambacho ni cha rangi nyekundu iliyo na weusi na weupe wa kutupiatupia. Kingine ni *Kisutu cha Wachinja Waume* ambacho ni rangi ya bluu kwa weusi. Inasemekana kuwa kanga za kisutu za mwanzo hazikuandikwa chochote. Kwa sasa, viko visutu vya rangi nyingine lakini visutu vinavyovaliwa na maharusi ni hivyo viwili.

Kanga za kisutu ni zenye kuenziwa sana toka hapo zamani. Hazikuwa zinavaliwa na mtu yeyote tu ambaye hajaolewa, bali huvaliwa na bibi harusi wakati wa kuoshwa. Wakati huu huvaa kisutu kutoka upande wa kwao. Baada ya kuoshwa, huvaa kisutu kinachotoka kwa mume. Hupelekwa chumbani kusubiri mume kuingia ndani akiwa amevishwa kisutu cha bi harusi. Kanga yenye weupe mwingi huvishwa bi harusi siku ya kwanza (wakati wa kuingia ndani). Siku ya tatu, katika fungate, huvishwa kisutu cha wachinja waume (tazama picha Na. 2 hapo juu).

Sababu za kutumiwa kwa kanga za kisutu katika matukio ya harusi ni kuwa, huwa zinapendezesha sana anapovaa mtu ikilinganishwa na kanga nyingine. Sababu ya pili ni kuwa, shanga anazovalishwa bibi harusi huwa na rangi maalumu ambazo ni nyeupe, nyekundu na nyeusi. Rangi hizi zinafanana na rangi ya kisutu cha bi harusi; hivyo, unapatikana mfanano unaovutia. Kwa vile huwa katika fungate, na nguo zinazovaliwa zaidi huko ni kanga (hasa kipindi cha zamani), hata watu wakiingia ndani, kuonana na bibi harusi au kunywa chai na maharusi, si rahisi kuonekana kwa rangi ya shanga hizo. Hivyo, inakuwa ni stara.

**Kanga katika Muktadha wa Mazishi**

Kanga pia hutumika katika muktadha wa mazishi. Katika muktadha huu, kanga hutumika kumfunika maiti mara tu anapokata roho. Zaidi, wakati wa kusafirisha maiti kanga huwa na maana maalumu kulingana na itakapofungwa. Iwapo atakuwa ni maiti wa kike, kanga hufungwa sehemu ya nyuma ya gari litakalobeba maiti. Kinyume chake, kanga hufungwa mbele ikiwa maiti ni wa kiume. Pia, kanga

hutumika wakati maiti anapooshwa. Baada ya kumalizika kwa zoezi la kuoshwa kwa maiti, kanga hizo huchukuliwa na watani wa marehemu na kwenda kuziosha.

Zaidi ya matumizi hayo, kizuka pia huvishwa kanga maalumu katika kipindi hicho cha uzuka. Kanga ambazo hutumika ni zenye kiza kama kanga za Magharibi pamoja na kanga za moto (zenye wekundu na weusi). Vilevile, katika mila na desturi za Wazanzibari, mtu anapofiwa na mtu wake wa karibu huoshwa. Mara nyingi, wenye kuchukua jukumu hilo ni jamaa wa mfiwa, mashoga zake au wifi zake. Hufanya hivyo kama njia ya kumfariji. Kanga mpya hutumika katika shughuli hii ya kumwosha mfiwa. Kanga za kiza na zenye majina ya kufariji hupendelewa zaidi.

**Umuhimu wa Kulinda Utamaduni katika Jamii**

Utamaduni ni mhimili katika maisha ya wanajamii. Kwa kawaida, mambo haya husababisha upekee wa jamii fulani, hivyo kuweza kutofautishwa na jamii nyingine. Hivyo basi, kutunza mila na desturi ni kutunza utambulisho wa jamii husika. Utambulisho ni jumla ya vigezo maalumu vinavyotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani ili kuonyesha kuwa liko tofauti na taifa jingine, kundi fulani liko tofauti na kundi jingine, au mtu fulani yuko tofauti na mtu mwingine (Msanjila, 2009). Vibainishi vya utambulisho ni kama vile lugha, mavazi, chakula, namna ya ujenzi wa nyumba, pamoja na amali za wanajamii.

Vilevile, kutunza mila na desturi ni kuendelea kuitunza historia ya jamii kwani vizazi vinabadilika na ulimwengu unabadilika kila uchao. Utandawazi unapoteza tamaduni nyingi kutokana na muathiriano wa jamii moja na nyingine. Hivyo basi jamii haina budi kulinda utamaduni wao kwa mustakbali wa vizazi vyao vijavyo.



Picha Na. 4: Kanga na mavazi mengine ya kiutamaduni katika jamii ya Zanzibar (lughatatu.wordpress.com).

## Hitimisho

Kila jamii ina tamaduni na kaida zake juu ya matumizi ya vitu mbalimbali kama vile, chakula, amali na hata mavazi. Kwa upande wa Zanzibar, kanga ni kitu adhimu sana. Kama ilivyo kwa watu wa Magharibi kumpelekea mtu ua, basi kwa Wazanzibari kanga hutumika kumpelekea mtu zawadi. Hivyo basi, makala hii imebainisha kwa kiasi gani vazi la kanga ni muhimu katika maisha ya jamii ya Wazanzibari.

## Marejeleo


Ali, H. & Kassim A. (2010). *Swahili Language and Culture*. Origin of Kanga April, *http://www.glcom.com/hassan/kanga - history.html # historia1*.

BAKITA (2016). *Kamusi Kuu*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Gadsby, J. (1995). *Looking at Writing on the Wall: A Critical Review and Taxonomy of Graffiti Texts.*

Hanby, J. & Bygott, D. (1984). *The History of Kanga. Retrieved on April 25, 2010. www.glcom.com/kanga - History.htlm*

Healey, J. (2010). *Sayings in East Africa Cloth. C:/Document and settings/pc/desktop/kanga/utamaduni – Fakta on Tanzania, kanga saying htm.*

Hongoke, C. (1993). *The Effect of Kanga Inscriptions, As a communication vehicle in Tanzania*. Dar es Salaam.

Mbarouk, S. (2011). Athari za Semi za Kanga kwa Jamii ya Zanzibar. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Mlacha S. & Hurskoinein, A. (1996). *Lugha Utamaduni na Fasihi simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila, Y. P., Kihore, Y. & Massamba, D. P. (2009). *Isimujamii*: Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam.

Wamitila, K. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.

Zawawi, S. (2007). Khanga – *The Cloth that Speaks*.From www.watatuse/product/info.php.